# TNMC Habari

Toleo No. 0017

TOLEO MAALUMU Januari, 2025

HALIUZWI www.tnmc.go.tz @tnmchabari


# Uzinduzi wa Baraza la 63 la TNMC

- ➜ Waziri Mhagama atoa Maelekezo ya utekelezaji kwa wajumbe wateule.
- ➜ Muuguzi Mkuu wa serikali apongeza Mchango wa Baraza liloisha Muda

Habari Uk. 01




## Matokeo Ya Mtihani Wa Usajili Na Leseni Yatangazwa, Ufaulu Ni 64%.




Habari Uk. 3-4

## Wauguzi, Wakunga Imarisheni Mawasiliano Kati Yenu Na Wagonjwa.



Habari Uk. 06

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania ni Mamlakaya Kisheria inayosimamia wanataaluma na taaluma za Uuguzi na Ukunga Tanzania chini ya Sheria ya Mwaka 2010 na kanuni zake (The Nursing and Midwifery Act, 2010) ili kuhakikisha huduma zinazotolewa na wauguzi na wakunga nchini Tanzania ni za kiwango kinachokubalika na salama kwa jamii.

# TIMU YA WAHARIRI

**MWENYEKITI**

Bi. Agnes Mtawa

**MHARIRI**

Mwakapiso Ndimmyake

**WARATIBU**

Irene Chilewa
Rose Mhando

**MSANIFU JARIDA**

Ezekiel Nyalusi

# Uzinduzi wa Baraza la 63 la Uuguzi na Ukunga

## ➡ Waziri Mhagama atoa Maelekezo ya utekelezaji kwa wajumbe wateule.

## ➡ Muuguzi Mkuu wa serikali apongeza Mchango wa Baraza liloisha Muda




Na. Ezekiel Nyalusi

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama, amelitaka Baraza jipya la Wauguzi na Ukunga Tanzania (TNMC) kusimamia maadili na kuwachukulia hatua kwa mujibu wa Sheria na taratibu wauguzi na wakunga watakaokiuka misingi ya Sheria na miiko ya taaluma za Uuguzi na Ukunga katika utoaji huduma kwa jamii.

Waziri Mhagama ameyasema hayo Januari 15, 2025 wakati akizindua Baraza jipya la 63 la Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania katika hafla iyofanyika Jijini Dodoma.

***"Baraza lenu lina kazi nyingi, miongoni mwa kazi zenu mnatakiwa kuhakikisha watumishi mnaowasimamia wanafanya kazi kwa weledi mkubwa ili kuwa na huduma zenye tija na ufanisi ili kupunguza utendaji kazi unasabaisha madhara na malalamiko kutoka kwa jamaii,"*** amesema Waziri Mhagama.

Aidha, Waziri Mhagama amelitaka Baraza hilo kuanzisha kanzi data inayoweza kufatilia wauguzi na wakunga wote nchini,waliyoajiriwa katika sekta ya umma,sekta binafsi na wasiyo na ajira. Hii itarahisisha ufuatiliaji wa mienendo yao na upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

***"Niwaelekeze Baraza, kuwa na mifumo mizuri inayohifadhi data za wauguzi na wakunga kuanzia walipo kwa sasa na mienendo yao, pia kuwatambua wauguzi na wakunga ambao hawana ajira ili kutengeneza mazingira mazuri ya kujiajiri kwa wataaluma hao,"*** amesema Waziri Mhagama.

Awali akimkaribisha Waziri wa Afya Mkurugenzi wa Idara ya Uuguzi na Ukunga kutoka Wizara ya Afya Bi. Ziada Sella, amelitaka Baraza hilo kusimamia mawasiliano pamoja na lugha za staha kwa wananchi wanaopatiwa huduma pamoja na kusimamia usajili wa wauguzi na wakunga sambamba na kutoa mafunzo mahala pakazi kwa wataalam hao.






KUTOKA UK.01

***"Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Baraza linaendela kusimamia mawasiliano na lugha nzuri kwa wataalam dhidi ya wananchi, eneo hili ni muhimu sana kwa sababu ndio matibabu yanaanzia hapo,"*** amesema Bi. Ziada

Kwa upande wa Mwenyekiti wa Baraza la Wauguzi na Ukunga Tanzania Prof. Lilian Msele amemshukuru Mh.Waziri wa Afya kwa kumwamini na kumteua kwa nafasi hiyo,na kwa kuwateua wajumbe wa Baraza hilo na kuahidi kutekeleza kwa vitendo maelekezo yote aliyoyatoa Waziri Mhe. Mhagama.

***"Nyuma ya mafanikio haya yote kuna mikono ya viongozi wetu kama Katibu Mkuu wa Serikali, wamekuwa mstari wa mbele kutushika mkono na kuhakikisha kila kwenye changamoto tunapata jawabu,"*** amesema Prof. Msele

Hata hivyo, Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Agnes Mtawa ameonesha furaha yake kwa kupatikana kwa Baraza jipya kitu kitakacho wezesha utekelezwaji wa haraka wa majukumu ya Baraza kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010 hapa nchini.

# Matokeo Ya Mtihani Wa Usajili Na Leseni Yatangazwa, Ufaulu Ni 64%.




Na. Ezekiel Nyalusi

Akitoa taarifa ya matokeo ya mtihani huo mapema tarehe 23 Januari, 2025, Jijini Dodoma, Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Agnes Mtawa, amebainisha kuwa, jumla ya watahiniwa 5125 walifanya mtihani huu, ambapo watahiniwa 3281 (64%) wamefaulu mtihani na watahiniwa 1844 (36%) hawakuweza kufikia kiwango cha ufaulu kinachokubalika.

Matokeo haya yanaonesha ongezeko la kiwango cha ufaulu kupanda kwa asilimia 13.3 ukilinganisha na matokeo ya mtihani uliofanyika Desemba, 2023 ambapo ufaulu wa jumla ulikuwa asilimia 50.7. Hali hii inaashira wahitimu waliweza kujibu maswali yaliyopima umahiri. Aidha, ufaulu katika ngazi ya stashahada umeongezeka kwa asilimia 11% ambapo kwa kipindi cha Desemba 2023 ufaulu ulikuwa asilimia 48%, Shahada ongezeko ni asilimia 27% ambapo ufaulu ulikuwa 72% .

**UCHAMBUZI WA UFAULU KWA NGAZI YA MAFUNZO.**

**SHAHADA YA UUGUZI**

Watahiniwa 537 wa ngazi ya Shahada ya Uuguzi waliofanya mtihani huu kutoka vyuo vikuu 15 vya ndani na nje ya nchi. Wanaume walikuwa 324(60%) na wanawake 213 (40%) . Ufaulu wa juu maksi 79% , Ufaulu wa chini maksi 48%, wastani 64%

**SHAHADA YA UKUNGA**

Watahiniwa 11 wa ngazi ya Shahada ya Ukunga waliofaulu mitihani huu kutoka vyuo viwili (2) vya Muhimbili na UDOM, kati yao 5(45%) wanaume walikuwa 6(55%) na wanawake



*KUTOKA UK.02.*

**SHAHADA YA UUGUZI KATIKA ENEO LA DAWA ZA USINGIZI NA GANZI**

Kati ya watahiniwa 14 wa kozi hii waliotoka Chuo Kikuu Muhimbili walifanya na kufaulu mtihani huu kwa vitendo na nadharia. Kati yao Wanaume 10 (71%) na wanawake 4(29%) watahiniwa wote walifaulu mtihani.

**D. STASHAHADA YA UUGUZI NA UKUNGA**

Ngazi ya Stashahada, jumla ya watahiniwa 4471 kutoka vyuo 103 walifanya mtihani waliofaulu 2655 kati yao Wanawake 1718 (59%) wanaume 937 (21%) Ufaulu wa juu maksi 72% ufaulu wa chini maksi 34% , wastani 51%

**E. ASTASHAHADA YA UUGUZI NA UKUNGA**

Jumla ya watahiniwa 92 wa ngazi ya Astashahada kutoka katika vyuo 41 walifanya mtihani huu ambapo Wanaume walikuwa 45 na wanawake 47. Watahiniwa 68 (74%) wamefaulu mtihani huu na watahiniwa 24 (26%) hawakufaulu.Ufaulu wa juu maksi 50% ufaulu wa chini maksi 20 , wastani 20%

Mtihani wa usajili na leseni ni kwa mujibu wa Sheria ya Bunge ya Uuguzi na Ukunga "The Nursing and Midwifery Act, 2010" Kifungu cha (6) (a) na (o) iliyounda Baraza la Uuguzi na ukunga nchini

Baraza linawapongeza wale wote waliofaulu na kupata sifa za usajili na leseni na kwa wale walioshindwa kufikia viwango vya ufaulu vinavyokubalika, watajulishwa muda wa kurudia mtihani huu.

# TAMA Yapata Ithibati Utoaji Wa Mafunzo Ya Kujiendeleza Kitaaluma (CPD)

Kwa niaba ya Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga, Mkunga Mbobezi na Mratibu wa Mafunzo ya Kujiendeleza Kitaaluma Bi.Mwajuma Mutabazi amekabidhi Cheti cha ithibati ya Moduli sita za mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma (CPD) eneo la huduma za dharura kwa wajawazito (Midwifery Emergency Skills Training) kwa Chama cha wakunga Tanzania (TAMA) ambapo amekitaka chama hicho kusimamia misingi ya kitaaluma huku akiahidi kuwa, Ofisi ya msajili ipo tayari kutoa ushirikiano.




Akipokea cheti hicho Jijini Dar es Salaam Rais wa TAMA Dkt. Beatrice Mwilike, amemshukuru Msajili kwa kuendelea kutoa ushirikiano na kuhakikisha Moduli za mafunzo zinazowasilishwa katika Ofisi yake zinafanyiwa kazi kwa wakati hivyo kurahisisha utekelezwaji wa mafunzo yenye lengo la kuwawezesha wataaluma wa kada ya Ukunga kupata maarifa mapya yatakayowawezesha kuendelea kutoa huduma bora kwa jamii hususani katika eneo la Mama na Mtoto.

Kwa upande wake, Katibu Mkuu wa TAMA Bwana Nicodem Komba, ameshukuru ushirikiano ulipo baina ya chama hicho cha kitaaluma na mamlaka ya usimamizi Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania.

Naye mshauri wa huduma za Ukunga kutoka TAMA Bi. Martha Rimoy, pamoja na Katibu Mwenezi wa chama hicho Bi. Agness Nduguru, kwa pamoja wameshukuru kupata cheti hicho huku wakiahidi kutoa mafunzo bora ambayo yamethibitishwa na Baraza kwa wakunga wote nchini ambayo licha ya kutoa huduma zenye viwango pia yatawaongezea alama wakati wa uhuishaji wa leseni zao.

# Wauguzi Na Wakunga Wakumbushwa Juu Mafunzo Ya Kujiendeleza Kitaaluma (CPD).




Na. Ezekiel Nyalusi

Akizungumza na TNMC Habari Ofisini kwake Jijini Dodoma, Mkurugenzi wa Maendeleo ya taaluma TNMC Bi. Happy Masenga, amesema,

***"Mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma ni mchanganyiko wa shughuli mbalimbali za mafunzo anayopata mtaaluma ili kujenga umahiri na kuimarisha uwezo wake wa kutoa huduma bora kwa kujifunza kila siku mambo mbalimbali katika eneo la kazi kutokana na uhitaji, changamoto zilizopo au uwepo wa mambo mapya (updates) katika taaluma na huduma kwa ujumla"*** amesema Bi Massenga

Bi. massenga ameongeza kuwa, mafunzo hayo yameandaliwa ili kuwawezesha wanataaluma kuwa na maendeleo endelevu ya umahiri wa taaluma ikijumuisha kurekebisha changamoto zinazofanywa na wataalamu kwa sababu ya kukosa umahiri, ujuzi duni na mtazamo usiofaa dhidi ya taaluma na Makosa mengine yanatokana na uwepo wa teknolojia mpya katika huduma za Afya ambayo watendaji hawakujifunza.

Kwa Upande wake msimamizi wa Mafunzo hayo Bi. Mwajuma Mutabazi, amebainisha umuhimu wa mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma CPD kuwa ni kukidhi mapungufu yaliyobainishwa katika ujuzi na maarifa ya mtaaluma binafsi na taasisi kwa ujumla, kumwongezea Muuguzi na Mkunga maarifa, ujuzi pamoja na kumpa mtazamo mpya (Knowledge, Skills and Attitudes) katika utoaji wa huduma, Kumwezesha Mtaaluma kutoa huduma bora kwa wateja wake zinazoendana na wakati.

Amezitaja faida nyingine kuwa ni kuwezesha wataaluma kukabiliana na changamoto mbalimbali za kuibuka kwa magonjwa, mabadiliko ya tabia nchi na ukuaji wa haraka wa sayansi na teknolojia, kuinua kiwango cha kufiriri na kufanya maamuzi ya kisayansi katika utoaji wa huduma ambao, humsaidia mtaaluma kukidhi takwa la Kisheria na kuweza kuhuisha leseni yake.




***"Muda wa Mafunzo ya kujiendeleza yamegawanyika katika sehemu tatu ambapo alama 2- 40 zimetolewa moja, Mafunzo ya muda mfupi kuanzia saa moja mpaka mwezi Pili, Mafunzo ya muda wa kati kuanzia miezi mitatu hadi sita***
***Tatu ni Mafunzo ya muda mrefu kuanzia mwaka mmoja na kuendelea"*** alisema Bi Mwajuma

Mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma CPD ni takwa la kisheria kwa wataalamu ili kuwa na maendeleo endelevu ya umahiri wa kitaaluma kwa mujibu wa Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya Mwaka 2010 na Kanuni yake Kifungu cha 6 (28)(1) cha Kanuni ya mafunzo ya mwaka 2010 (The Nursing and Midwifery Training Regulations, 2010)

# Msajili TNMC; Wanachuo Zingatieni Usajaili wa Awali (StudentIndexing)



Na. Ezekiel Nyalusi

Msajili wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania Bi. Agness Mtawa, amewataka wanafunzi wote wa kada ya Uuguzi na Ukunga nchini kuhakikisha wanakamilisha usajili wa awali (Student Indexing) ili kuweza kutambulika na mfumo wa Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania tangu wakiwa vyuoni.

Msajili Mtawa, ameyasema hayo wakati wa kikao kilichoombwa na chama cha wanachuo wa taaluma ya Uuguzi na Ukunga wa Chuo Kikuu cha St. John kilichopo Jijini Dodoma na kufanyika chuoni hapo.

***"Naomba niwaeleze kwa nini ni muhimu kukamilisha usajili wa awali, kwanza ni Kurahisisha ufuatiliaji wa wanafunzi waliodahiliwa na wanaoendelea na mafunzo katika vyuo, Kurahisisha mchakato wa usajili baada ya kuhitimu mafunzo, Hurahisisha ufuatilia wa maendeleo ya mafunzo vyuoni na kutoa takwimu ya wanafunzi wanaostahili kufanya mtihani wa leseni na usajili, kujua hali ya udahili wa wanafunzi katika vyuo vya Uuguzi na Ukunga"*** alisema Bi. Mtawa.

Msajili amesisitiza kuwa, Usajili wa awali (student indexing) si kwa ajili ya kupata kibali cha kufanya mtihani wa Usajili na Leseni tu bali ni zoezi muhimu linalomwezesha mwanafunzi kufanyiwa uhakiki wa sifa za kujiunga na masomo ya Uuguzi na Ukunga kisha kupata au kutopata kibali cha kuendelea na masomo hayo.

Kwa upande wake Afisa Mafunzo Bwana John Kafumu, amebainisha kuwa, wadahiliwa ambao taarifa zao hazijawasilishwa Baraza hawataweza kufanya usajili huu, Sambamba na hilo, mwanachuo aliye kamilisha usajili wa awali atapata kadi ya usajili wa awali (indexing card) itakayotumika kwa kipindi chote cha uanachuo na wakati wa mtihani wa Usajili na leseni.

***"Utaratibu wa kujisajili ni kuingia kwenye tovuti ya Baraza kwa kuandika neno TNMCIS au www.tnmc.go.tz Baada ya kuingia kwenye ukurasa huu wa Baraza bofya TNMCIS login utaona ukurasa huu na Bofya "click here to register" kwa waombaji wapya ambao hawana akaunti Baraza Kwa sasa maombi mengi kupitia Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania yanafanyika kwa njia njia mtandao. Hivyo mwombaji anawajibika kuchagua ombi sahihi kwa wakati huo kama ambavyo ukurasa hapo juu unavyoonyesha"-alisema Bwana Kafumu***

Bwana Kafumu aliongeza kuwa, kwa wanafunzi ambao tayari wanaakaunti kwenye mfumo wa Baraza hawatakiwi kujisajili tena bali wanatakiwa kuingia moja kwa moja kwenye mfumo (login) kwa kuweka barua pepe na nywila zao kisha kuendelea na kukamilisha maombi.

Nao wanafunzi wa kada ya Uuguzi na Ukunga kutoka Chuo cha St. John, Frola Amosi na Thomas Mwita, wametoa shukrani zao za kipekee kwa Msajili kwa kukubali kufika na kutoa semina juu ya usajili wa awali kwao

# Wauguzi, Wakunga watakiwa Kuimarisha Mawasiliano Kati yao na Wagonjwa



Na. Ezekiel Nyalusi

**Wauguzi na wakunga wametakiwa kuimarisha mawasiliano bora na wagonjwa ili kuboresha utoaji wa huduma za Afya, kuanzia huduma za Afya ngazi ya msingi.**

Hayo yamesemwa Januari, 18 2024 na Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Uuguzi na Ukunga kutoka Wizara ya Afya, Bw. Paul Magesa, wakati akihitimisha kikao kazi cha kupitia na kuhakiki kitita cha huduma staha zinazozingatia utu, heshima, na maadili.

***"Vipaumbele vya Wizara ya Afya ni kuhakikisha ubora wa huduma kwa wananchi, ambapo mawasiliano na lugha ya staha ni sehemu muhimu ya malengo haya. Mawasiliano ya staha ni sehemu ya miongozo ya maadili kwa wauguzi na wakunga, kwani yanachangia katika kujenga uaminifu na kuboresha uhusiano na wagonjwa, "*** amesema Bw. Magesa.

Magesa amesema, wauguzi na wakunga wanachangia kwa kiasi kikubwa katika utoaji wa huduma za Afya, wakiwa ni asilimia 60 ya watoa huduma katika sekta hii



Kwa kuwa wao ndio wanaotangamana zaidi na wagonjwa kila siku, mchango wao ni muhimu sana katika kuboresha hali ya Afya ya jamii.

***"Ili kuboresha mawasiliano kati ya wauguzi na wagonjwa, ni muhimu kuweka nyenzo zinazowawezesha wauguzi kuwahudumia wagonjwa,"*** amesema Bw. Magesa.

Hiki kitita kinajikita katika miongozo ya maadili kwa wauguzi na wakunga kazini, ambapo mawasiliano bora na uwazi ni muhimu katika kuboresha huduma za Afya.

# Mkurugenzi (WHO) Atembelea Kituo Cha Afya Makole - Dodoma, Serikali Yaahidi Ukarabati.



Na. Ezekiel Nyalusi

Serikali kupitia Wizara ya Afya imetenga zaidi ya Shilingi Bilioni Saba za kitanzania kwa mwaka wa Fedha 2024/25 kwa lengo la kukarabati Kituo cha Afya Makole ili kiwe na majengo yenye hadhi ya ghorofa hali itakayo ongeza tija katika utoaji huduma hususani katika eneo la Afya ya Mama na Mtoto.

Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama, amesema hayo Januari 20, 2025 alipofanya ziara kwenye Kituo cha Afya Makole akiwa ameambatana na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Dkt. Tedros Ghebreyesus, aliyefika kujionea huduma zinazotolewa katika kituo hicho kilichopo katikati ya Jiji la Dodoma.

***"Tumekuja hapa Kituo cha Afya Makole na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Dkt. Tedros Ghebreyesus, kwa lengo la kuona juhudi za Serikali za katika utoaji huduma za Afya hususani kwenye kuokoa vifo vya Mama na Mtoto, lakini pia miradi ambayo Serikali inaendelea kuisimamia,"*** amesema Waziri Mhagama

## Tsh.Billion 7

*Wizara ya Afya imetenga zaidi ya Shilingi Bilioni Saba za kitanzania kwa mwaka wa Fedha 2024/25 kwa lengo la kukarabati Kituo cha Afya Makole*

Aidha, Waziri Mhagama amesema huduma za msingi ambazo zitakuwa zikitolewa katika kituo hicho ni pamoja na huduma ya uzazi ili kuendelea kuokoa vifo vya mama na mtoto kwani hadi sasa Serikali imepunguza vifo hivyo kutoka 556 kwa vizazi hai 100,000 hadi 104 kwa vizazi hai 100,000 ndani ya kipindi cha miaka minne.

Kwa upande wake Mganga Mkuu wa Jiji la Dodoma, Dkt. Pima Sebastian, ameishukuru Serikali kwa kutoa fedha hizo kwa lengo la kukarabati kituo hicho.

***"Tunashukuru kwa kutembelewa na ugeni huu mkubwa ukiongozwa na Waziri wa Afya Mhe. Jenista Mhagama, aliyeambatana na Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Afya Duniani Dkt. Tedros Ghebreyesus, kuja kuona huduma zinazotolewa katika kituo chetu cha afya Makole,"*** amesema Dkt. Pima

# HABARI PICHA MWEZI JANUARI




*Bi. Mwajuma Mutabazi amekikabidhi Cheti cha ithibati ya Moduli sita za mafunzo ya kujiendeleza kitaaluma (CPD) kwa Chama cha wakunga Tanzania (TAMA)*




*Msajili wa TNMC Bi.Agnes Mtawa ktk picha ya pamoja na viongozi wa chama cha wanafunzi wa kada ya Uuguzi na Ukunga chuo cha St.John Dodoma baada ya semina juu ya usajili wa awali.*



*Msajili wa TNMC Bi. Agnes Mtawa ktk picha ya pamoja na Menejimenti ya TNMC baada ya kutembele eneo la ujenzi wa Ofisi za TNMC zilizopo Eneo la Medeli jijini Dodoma.*




*Wanafunzi wa Chuo cha St.John Dodoma wakipata Semina kutoka TNMC Juu ya Usajili wa awali.*









JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA AFYA
BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA TANZANIA

**TAARIFA KWA UMMA**

**UHUISHAJI WA LESENI ZA UUGUZI NA UKUNGA ZILIZOKWISHA MUDA TANGU MWEZI DISEMBA 2024**

***12.02.2025, Dodoma.***

Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania **(TNMC)** linawakumbusha wauguzi na wakunga wote nchini kuhuisha leseni zao zilizokwisha muda wake tangu mwezi Disemba 2024, kwani kuendelea kutoa huduma pasipokuwa na leseni hai ni kosa kisheria kwa mujibu wa Kifungu cha 38(i) (a) (b) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga.

Kwa mujibu wa Kifungu tajwa hapo juu, Muuguzi au Mkunga ambaye atatoa huduma pasipokuwa na leseni hai, ataondolewa kwenye daftari la usajili au kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria.

**Aidha,** uhuisahaji wa leseni unakwenda sambamba na Mafunzo ya kujiendeleza kazini (CPD) ili kuboresha huduma za Uuguzi na Ukunga, waajiri wote mnakumbushwa kufanya uhakiki wa wauguzi na wakunga mliowaajiri ili wawe na leseni hai za kitaaluma.

**Hata hivyo,** waajiri wote mnakumbushwa kuwa kutoa ajira kwa muuguzi au mkunga asiye na leseni hai ni kosa kisheria chini ya Kifungu cha (44) cha Sheria ya Uuguzi na Ukunga ya mwaka 2010 kwani kufanya hivyo unaweza kushitakiwa na kutozwa faini kwa mujibu wa Sheria.

Ndimmnyake Mwakapiso
*Mkuu wa Kitengo cha Uhusiano na Mawasiliano TNMC*

@tnmchabari
+255 737 96 26 91
Ofisi ya Msajili TNMC
S. L. P 1736 Dodoma -Tanzania
Simu +255 736 00 60 60
Barua pepe: info@tnmc.go.tz

# UKURASA WA TANZIA

**Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania limepokea kwa Masikitiko vifo vya wauguzi na wakunga wenzetu waliotangulia mbele ya haki Mwezi Januari, 2025, baada ya kumaliza kazi ya hapa Duniani, Mwenyezi Mungu azilaze Roho zao Mahali pema Peponi AMENI.**



**JINA:** ROSEMARY ANTON CHILEMBA
MSTAAFU
**WILAYA:** LIWALE
**MKOA:** LINDI



**JINA:** FANUEL BATHOLOMEO
**KITUO:** HOSPITALI YA RUFAA
**MKOA:** GEITA

# MAFUNZO

## KWA VITENDO KAZINI (CPD)

Kwa Watumishi Wanaotoa Huduma Vyumba Vya Upasuaji

**HOSPITALI YA RUFAA YA MKOA MAWENI-KIGOMA**




**MUWEZESHAJI:**
BI. SALOME KASSANGA
Mtaalamu Mbobezi chumba cha Upasuaji - **KUTOKA TNMC**

03-16 Februali 2025

Hospitali ya Rufaa ya Mkoa Maweni -Kigoma

JARIDA LA BARAZA LA UUGUZI NA UKUNGA

Limeandaliwa na Kitengo cha Uhusiano
Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania
S.L.P 1736 DODOMA , **Simu: 0736 00 60 60**
Barua Pepe:Info@tnmc.go.tz
Tovuti:www.tnmc.go.tz

HAKI ZOTE ZIMEHIFADHIWA